# JE INALETA TOFAUTI NI KANISA GANI UNASHIRIKI?

JE

INALETA

TOFAUTI

NI

KANISA

GANI

UNASHIRIKI?

Kwa utatanishi mwingi wa mashirika ya Kikristo na clini mbalimbali, pamaja na makanisa yanayoitwa majina mbalimbali na hata njia za kuabudu pamoja na mafunzo, swali huweko "Je inaleta tofauti ni kanisa gani unashiriki?  Unafikiria nini?

Tafadhali fungua ukurasa, na kwa pamoja hebu tukayachunguze mafungu machache ambayo yatatuelekeza kwa maji ya hili swali."

*"Angalieni mtu asiwadanganye. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema. Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi."*

Katika Mathayo 24:4-5, Jesu atwambia kuwa "wengi" watawadangarya wasiojua, na basi kwa hiryo watawapotosha wengi kutoka kwa injili ya kweli, pia twasoma katika Mathayo 7:13-14:

*"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlanga ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache."*

Kwa onyo hii kutoka kwa Mungu kuhusu wengi ambao watadanganya na watakaodanyanywa, na kuhusu mlango mwembamba na njia nyembamba, hakika ona uzuri wa kuitafuta njia hiyo nyembamba.

Kwa kuchukulia kwamba zote twaamini kuwa kuna maisha baada ya kifu--maisha ya milele--ni muhimu tutafute njia ya kuyapata hayo maisha na uzima wa milele; kwa kutofanya kama wafanyao wengi: wanabaki bila matayarisho sababu wameingia katika mlango mpana. Kumbuka kwamba sio ukweli wote ni wa kupendeza, sana sana ukiwa ni wa tofauti kutoka kwa ule ukweli tuliofunzwa awali. Jesu alituonya dhidi ya kufuata tamaduni katika Marko 7:9:

*"Akawaambia, vema! Mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu."*

Hapa Marekani, tuna mahali karibu mia mbili na hamsini ya vikundi na makanisa ya Wakristo, ambayo husingisia kwamba wametumwa na Mungu kuihubiri injili na kuwaokoa wenye dhambi, na yote hayo hufunza mafunzo tofauti. Wengine kufunza kwamba twastahili "kumfuata na kuamini katika jina la Bwana." Lakini hata shetani huamini katika jina la Bwana! Hakuna makundi mawili ambayo hufundisha mafunzo sawa, kwa hiryo hayawezi kuwa sawa yote. Moja au zaidi lazima yawe na upotevu. Yote jangekubali yangeungana, lakini sasa yanatofautiana; na ajabu ni kwamba, yote husingisia kuwa na ukweli.

Sasa ewe msomaji, ikiwa wewe ni mshiriki wa kanisa ya "Methodisti," una haja gani kwa kutoshiriki "Baptist"? Ikiwa unashiri "Baptist" una haja gani kwa kutoshiriki "Presbyterian"? Ushawai kufikiria swali la namna hii? Ama wewe ni mmoja kati ya

wasemao, "Haaileti tofauti ni kanisa gani unashiriki; zote twaelekea mbinguni lakini kwa njia tofautitofauti."?

Jesu alisema:

*"Amin, amin, nawaambieni, yeye asiyeingia mlangoni katika zizi la kondoo, lakini akwea penginepo, huyo ni mwivi naye ni mnyanganyi."  (Johana 10:1)*

Masiah wetu alifunza kwa miaka kadhaa, na alikatali wa mara nyingi kwa sababu aliongea wazi mafunzo yake.  Alimwambia Nikodmo wazi kwamba:

*"...mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu...mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." (Johana 3:3, 5)*

Hiyo ni lugha ya mkazo!  Hakuna njia mbili za kwenda mbinguri kulingana na maneno hayo.  Tunawapata "Wakristo" wengi na wazuri wasio ona maana ya kubatizwa.  Ijapo Bibilia yazingatia hiryo.  Mtu aweza kuotea.

Sasa kwa kumfuata Bwana katika batizo:

*"Johana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele." (Johana 3:23)*

*"...wote walibatizwa katika mto Yordani..." (Marko 1:5)*

*"...wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza." (Matendo 8:38)*

*"Naye Jesu, alipokwisha kubatizwa, mara akapanda kutoka majini..." (Mathayo 3:16)*

*"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo..." (Warumi 6:4)*

*"Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo, na katika huo mkafufuliwa pamoja naye..." (Wakolosai 2:12)*

Basi kulingana na Bibilia, hebu natuone mahitaji ya batizo:

1. Lazima kuweko na "maji."

2. Inahitaji "maji mengi."

3. Yafaa tuingie "chini majini."

4. Ni kuzikwa au kutumbukizwa ndani ya maji.

5. Baada ya "kuzikwa" ndani ya maji, "tunafufuka" tena na kuja "nje ya maji."

Sasa kwa kufananisha, hebu na tufuatilie njia za wale wanaobatiza kwa kutilia maji:

1. Maji? Ndio.

2. Maji mengi? La.

3. Huenda chini majini? La.

4. Je mtu huyo huzikwa majini? La.

5. Mtu huyo hufufuka tena na kutoka ndani ya maji? La.

Twaona kuwa, njia ya kutilia maji yakubalika mara moja tu: Utumiaji wa maji. Hakika haiwezi kuwa ya kweli, kwa hivyo ni mbaya.

Twapata kuwa makanisa mengine humpa mtu anayetaka kubatizwa uhuru wa kuchagva njia moja ya kubatizwa kati ya tatu: yaani kutiliwa maji kumwagiwa maji au kutumbukizwa ndani ya maji. Ni upoteuu kabisa kutoka kwa njia iliyo nyembamba na laini! Lakini mtume Paulo atuonya:

*"Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo." (2 Timotheo 4:3-4)*

*"Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana baba na mwana pia. Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu." (II Johana 9-10)*

Ufalme wa Mungu umetengenezwa kwa nini? Webster asema kwamba ufalme ni mahala "anapotawala mfalme." Kuwa na ufalme, cha muhimu lazima kuweko na watu wa kutawalwa, na mfalme pamoja na wadogo au wafuasi ambao wako chini yake. Hivyo, kwa kupata vitu vinavyoufanya "ufalme wa mbinguni" hebu natuangalie Bibilia:

1. Mfalme: Kristo ndiye kichwa, na kwa yeye, vitv vyote vimo. (Wakolosai 1:17-18)

2. Wafuasi: "Na akawapa wengine, mitume; na wengine, manabii; na wengine, waandishi wa injili (wainjilisti); na wengine, wapasta na waalimu;" (Waefeso 4:11); Maaskofu na mashemasi (Wafilipi 1:1); "wakawachagulia wazee katika kila kanisa (Matendo 14:23).

Kristo alipoianzisha kanisa yake, aliwafanya mitume wake kama viongozi wa roho ya kanisa asipokuwemo.  Kuhusu wafuasi wake, twapata agizo lifuatalo:

*"Na hakuna mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni." (Waebrania 5:4)*

Tunavyosoma katika Kutoka 28:1, twapata kuwa hakika Haruni aliitwa na Mungu, ufunuo aliopewa Musa; hii na iwe mtindo kwa kanisa la Kristo milele, kwa:

*"Jesu Kristo ni yeye yule, na leo, na hata milele." (Waebrania 13:8)*

Kwa kutumia Bibilia, tena hebu natuangalie ufalme huo umeunganishwa na nini:

*"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuynena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msini tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kua na imani kwa Mungu, na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milel." (Waebrania 6:1-2).*

Kwa mafunzo sita muhimu, twapata kwamba Bwana hupeana vipawa tisa vya Kiroho kwa yeyote atakaye:

*"Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la "hekima"; na mwingine neno la "maarifa," apendavyo yeye Roho yule; mwingine "imani" katika Roho yeye yule; na mwingine "karama za kuponya," katika Roho yule mmoja; na mwingine "matendo ya miujiza";  na mwingine "unabii"; na mwingine "kupambanua roho" mwingine "aina za lugha," na mwingine "tafsiri za lugha." (I Wakorintho 12:8-10)*

Tayari tumeambiwa kwamba bila huruma au upendo, hivi vipawa vyote ni bvre. Ikiwa kimoja kati hivi vitu kimepoa, au kitapoa, basi ni sababu ya kutoamini; ikiwa miujiza imepoa, ndivyo imani pia imepoa.  Sisi wa Kanisa la Kristo twaweza kushuhudia kwamba haya mambo hayajapoa.

Tayari tumeonyesha kindani kuwa inaleta tofauti ni kanisa gani twaweza kushiriki ili ituongoze katika kwenye "mlango unaotakikana," njia ya kipekee kwa uzima wa milele, na hiyo ndiyo pekee kamilifu katika misingi yake ya kiroho bila kitu kvachwa nje, au bila kuongezwa, ambacho hakitakiwi kwa njia kamili Jesu alioianzisha Kanisa yake hap mwanzo.

Kuna vitu viwili ambavyo mtafutaji wa kweli lazima avifanye, invyosemwa katika Yakobo 1:5 na II Timotheo 2:15:

*"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa."*

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."*

Mbali usimuachie muhubiri yeyote uhuru wa kukufikiria. Fikiri na ujifunze peke yako. Ona kama muhubiri ako sawa; yuaweza kuwa sawa, lakini wajuaje?

Sisi ni "Kanisa ya Kristo," na mahediquota katika (Temple Lot in Independence, Missouri). Wewe pamoja na familia yako mna mwaliko ulio wazi kuhudhuria huduma katika kanisa yeyote kote ulimwenguni. Kwa maelezo zaidi andika kwa:

Kanisa ya Kristo (Temple Lot)
S.L.P. 472
Independence, Missouri 64051

au tembelea (our visitor's center at the southwest corner of River and Lexington in Independence).